# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu,
70490 Mjini Magharibi,
S.L.P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 2242000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA KAMATI YA BAJETI YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUWEKA MASHARTI YA UTOAJI WA LESENI, KUDHIBITI NA KUSIMAMIA BIASHARA YA HUDUMA NDOGO NDOGO ZA FEDHA KWA AJILI YA KUDUMISHA UTULIVU, USALAMA NA UBORA WA HUDUMA NDOGO NDOGO ZA FEDHA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kuanza hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuendelea kutupa neema yake ya uhai, afya na uzima tukaweza kuendelea na utekelezaji wa majukumu yetu katika Baraza hili.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa dhati kabisa nakushukuru wewe pia kwa namna unavyoliendesha Baraza hili ukishirikiana na wasaidizi wako, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Baraza ambao nyote kwa pamoja mumekuwa mkiliendesha Baraza kwa weledi na umahiri mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Nachukua fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili kutoa Maoni ya Kamati kuhusiana na Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utoaji Leseni, Kudhibiti na Kusimamia Biashara ya Huduma Ndogo Ndogo za Fedha kwa ajili ya kudumisha Utulivu, Usalama na Ubora wa Huduma Ndogo Ndogo za Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kukamilika kwa Hotuba hii kumetokana na mashirikiano makubwa ya Wajumbe wa Kamati yangu. Naomba uniruhusu niwatambue kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan | Makamo Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Asha Abdalla Mussa | Mjumbe |
| 4. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 5. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe |
| 6. Mhe. Rukia Omar Ramadhan | Mjumbe |
| 7. Mhe Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |
| 8. Mhe. Zawadi Amour Nassor | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** Pia naishukuru Sekretarieti ya Kamati yenye makatibu wanne ambao hutusaidia kwa karibu katika kufanikisha majukumu yetu tuliyopangiwa. Naomba pia uniruhusu niwatambue kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Abass Vuai Moh’d | Katibu |
| 2. Ndg. Asha Said Mohamed | Katibu |
| 3. Ndg. Husna Rajab Othman | Katibu |
| 4. Ndg. Shaib Fadhil Shaib | Katibu |

## UCHAMBUZI WA MSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Bajeti ilipokuwa inaupitia Mswada huu, ilipata fursa ya kukutana na wadau wa huduma ndogo za fedha,

Wanasheria wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na uongozi pamoja na Watendaji wa Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango. Kwa kiasi kikubwa ufafanuzi na maoni yao yamesaidia katika kuikamilisha kazi hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta mswada huu katika kipindi sahihi kwani utasaidia katika kusimamia taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha, kwa kuhakikisha kuwa zinasajiliwa rasmi na kutekeleza majukumu yake kwa kufuata taratibu zilizowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Sheria hii, utasaidia kwa kiasi kikubwa kuweka misingi madhubuti na yenye ufanisi katika mfumo wa huduma ndogo za fedha nchini, ili kuchangia ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Sambamba na kupambana na vitendo vya kitapeli vilivyokithiri katika huduma hizi ndogo za fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa huduma ndogo za fedha hapa Zanzibar zinakabiliwa na mapungufu mbali mbali kama vile ukosefu wa mfumo wa sheria na kanuni za kusimamia taasisi ndogo za fedha zisizopokea amana na taasisi za fedha zisizo rasmi, kiwango cha chini cha uelewa wa masuala ya fedha kwa wananchi wetu, upungufu wa taarifa za sekta ndogo ya fedha, kukosekana kwa mfumo wa kumlinda mteja wa huduma ndogo za fedha, na kukosekana kwa chombo cha kuhifadhi taarifa za mikopo. Pamoja na hayo, Sheria hii itamuwekea mtoa huduma mazingira rasmi, bora, tulivu na salama ya kutoa huduma hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande mwengine, kumekuwepo na changamoto mbali mbali kuhusiana na uendeshaji wa utoaji wa huduma kwenye taasisi ndogo za fedha na uwezo wake katika kupunguza umaskini. Suala hili kwa

kiasi kikubwa linahusishwa na kutokuwepo kwa uwazi kwenye masharti ya ukopeshaji, viwango vya juu vya riba, utoaji holela wa mikopo na wateja kuwa na mikopo mingi inayosababisha limbikizo la madeni, na utaratibu mbovu wa ukusanyaji wa madeni.

**Mheshimiwa Spika,** Maendeleo ya mfumo wa fedha yanategemea utulivu wa sekta ya fedha nchini hasa katika utulivu wa mfumo wa taasisi ndogo za fedha, hivyo kuwepo kwa Sheria hii kutasaidia kufikia hatua hiyo pamoja na kuweka mazingira bora kwa taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekuwa ikitekeleza hatua mbali mbali za kuimarisha sekta ya fedha nchini ili kukabiliana na changamoto katika sekta hiyo kwa kuweka misingi imara yenye kukuza ushindani halali na utendaji makini.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Kifungu cha 5 kinachoelezea madaraja ya watoa huduma ndogo za fedha na Kifungu cha 8 kinachoelezea mabadiliko ya watoa huduma ndogo za fedha, Kamati katika vifungu hivi inashauri kwamba, wakati wa utungaji Kanuni kueleza wazi utaratibu pamoja na sifa zitakazotumika wakati wa kupanda au kushuka kwa madaraja ya watoa huduma ndogo za fedha ili kuwapa uelewa watoa huduma ndogo za fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Kifungu cha 10 ambacho kinaelezea muundo wa viwango vya riba au tozo, pamoja na kupewa fursa mtoa huduma ndogo za fedha kuweka muundo wa viwango vya riba, faida au tozo kwa lengo la kupata fedha kwa ajili ya shughuli za uendeshaji, Kamati inaishauri Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango, katika Kanuni zitakazotungwa kuwekwe utaratibu maalum wa kuwadhibiti watoa huduma ndogo za fedha katika kuweka viwango vya riba au tozo kwa kuweka viwango vinavyokubalika na visivyoleta athari kwa pande zote mbili.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa, naomba ifahamike kwamba, Kamati ilipokuwa inapitia Mswada huu, pamoja na mambo mengine ilibainisha marekebisho mbali mbali yakiwemo ya lugha, mpangilio wa baadhi ya vifungu na makosa ya kiuandishi ambayo yote kwa pamoja yamependekezwa kurekebishwa kama yalivyoambatanishwa katika hotuba hii.

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kumalizia, Kamati inaitaka Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango kuharakisha utungaji wa Kanuni ili mswada huu utakaposainiwa na Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria uweze kutekelezeka. Aidha, kukamilika kwa utungaji wa Kanuni hizo kutapelekea kuwepo kwa usimamizi mzuri wa sekta ndogo ya fedha nchini ambayo ni muhimu sana katika kupunguza umaskini, kukuza uchumi na kuwepo kwa uwazi katika uendeshaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Ni mategemeo ya Kamati yangu kwamba, Sheria hii itasaidia kuongeza uwazi, ufanisi, na usalama katika huduma ndogo za fedha, ambayo kwa kiasi kikubwa itachangia katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Ahsante,

……………………

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma,
Mwenyekiti,
Kamati ya Bajeti,
Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**